**MAELEKEZO YA UOMBAAJI WA SCHOLARSHIPS NA PASSPORT**

Hatua rahisi za kufanya maombi ya ufadhili wa masomo kwa ngazi zote i.e Bachelors, ,Masters na PhD.

1. Fahamu chuo kinachotoa programu unayotaka uisoma

   www.campuschina.org or www.csc.edu.cn/laihua.

   https://www.cscscholarship.org/subject-wise-university-list-under-csc

2. Ingia kwenye ‘Website’ ya chuo ulichokipenda na zielewe vizuri ‘admission process’ zake pamoja na kujua muda wa kufungwa kwa maombi ya ufadhili kupitia chuo hicho na aina za ufadhili katika chuo husika.

3. Zifahamu ‘Agency number’ za vyuo mbalimbali, hizi zitakusaidia kujaza utapoanza maombi yako;

   https://www.cscscholarship.org/chinese-universities-agency-number-list.html

4. Fungua akaunti na anza maombi yako kwa kujaza taarifa zako binafsi pamoja nyinginezo zihusuzo historia ya elimu yako;

   http://studyinchina.csc.edu.cn/

5. Kupitia namba (2 & 4) utafanikiwa kupata fomu mbili (Specific University application form + CSC application form); na kupata vyuo na kujua course unazohitaji kusoma.

NB: Fomu Hizi mbili na documents nyingine ambazo zitatajwa kwenye ukurasa wa mwisho wa ‘CSC application form’ utatakiwa uzitume kwenye anuani ya chuo husika Japo vyuo vingine utapaswa usubiri wakupe taarifa ikiwa wanahitaji uwatumie au vinginevyo (Ukiingia katika website ya chou husika utakuta maelezo ya maombi na namna ya kufanikisha maombi).

Tofauti ya Category A&B

CATEGORY A

Hii uomba kupitia TANGAZO LA WIZARA ya ELIMU na MOFCOM kupitia tangazo la website ya UTUMISHI. Unaingiza agency number INAYOTOLEWA NA WIZARA/TANGAZO HUSIKA linalotolewa na wizara ya Elimu Tanzania au Utumishi. Then AUTOMATICALLY badala ya kuonekana jina la chuo itakuja jina la ubalozi wa Tanzania nchini China. Utajaza TAARIFA ZAKO KAMA FORM INAVYOKUELEKEZA.

KWA CATEGORY A, utajikuta unatumia ACCOUNT moja kuomba vyuo vitatu na UTAVIAINISHA VYUO HIVYO KWENYE NAFASI ULIYOELEKEZWA.

## CATEGORY B

Hii inahusika na maombi kupitia chuo husika moja kwa moja, Hivyo matangazo yake hupatikana katika website ya chuo husika. **Kwa sasa Category B inaruhusu chuo kimoja tu tofauti na awali ambapo ilikuwa vyuo 3.**

Hii category inakuhitaji kufungua account mpya yaani uwe na e-mail addresses 1 kwa ajili ya kufungulia account ya chuo kuombea chuo husika. e-mail address utakayoijaza ndani kwenye form inaweza kuwa 1 (kujirudia) for correspondence. Unaendelea kuijaza form kama inavyokuhitaji.

## MOFCOM SCHOLARSHIP

Tangazo la hii hutolewa katika website ya Utumishi

https://www.nationalmeritscholarships.com/mofcom-scholarship-in-china.html (Ila usiitumie kuomba mpaka matangazo yatolewe)

Hatua za awali za kujiandaa Kwa ajili ya baadae

Pia andaa documents 1_08 Soma Tasafic 06

1. Ukiingia kwenye website ya utumishi www.utumishi.go.tz utakuta tangazo na Zipped folder/Compressed folder lenye documents za application zote

2. Utajaza application form kwa kufuata maelekezo

Kila application inakuwa na form yake direct to chuo kwanza na kila package ina maelekezo yake. Wanakuambia jaza form, scan viambatanisho kisha utume kwa **email** yao. Wakivipata watakujibu.

3. wanakupa notification ***that you have to apply for CSC*** hapa utajaza csc category A. agency number utaweka ya ubaloz wetu Tz (Utapewa katika Tangazo husika)

**Note:** Mara ya mwisho walikuwa na vyuo separate 39 na watanzania zaid ya 90 walipata nafasi**,** kwaiyo tusubiri utumishi watoe, watatoa na **agent number** ambayo ni ubalozi wetu

## LIPIA APPLICATION FEE KWA MASTERCARD (KWA VYUO VINAVOKUHITAJI KUFANYA HIVYO)

1. Lipia kwa Bank A/C

Maelekezo: Nenda bank weka hela katika Acount yako yenye uwezo wa kufanya International transactions (malipo ya mtandao)

Nenda reception waonyeshe online application eneo la pay fee; wataona money order watafanya transaction vizuri. Mtu yeyote aweza kukulipia kwani kinancholipiwa ni application number via money order number na sio nani kalipa.

2. Pia kwa Simu

Jaribu kwa M-Pesa MasterCard kwa utaratibu huu

i. Unaingia kwenye menu ya M-Pesa (*150*00#)

ii. Ingia no. 4 (lipa kwa M-Pesa)

iii. Ingia no. 6 (M-Pesa MasterCard)

iv. Ingia no. 1 (Tengeneza Card)

Baada ya hapo utapata ujumbe wenye M-Pesa MasterCard Namba yako na expire date yake.

NB: Note pembeni taarifa:

## MAELEKEZO MAFUPI YA KUOMBA PASSPORT

Kuhusu suala la kuomba passport kwa urahisi sana na hii njia itakusaidia kuepuka vikwazo vinavyoweza kujitokeza.

Kwanza, kabisa unajijua unataka passport, silaha namba moja ya kuweza kupata hiyo kitu ni lazima uwe na kitambulisho cha taifa m.f NIDA, Leseni, kitambulisho cha mpiga kura.
kama hauna id ya taifa basi itafute hiyo kwanza maana bila hiyo huwezi kuendelea na mchakato wala kuanza. Na sasa hvi mchakato wa ID ya Taifa kidogo umerahisishwa hata kama hauna ID mkononi unaweza kuombea kwa ile namba ya ID utakayopewa pindi ukisubiria kadi yako ya Taifa.
Pili, Hauhitaji uwe na admission letter wala barua ya mualiko wala udhamini,

Kama unaomba passport, fuata hatua ifuatazo;

- Kutoa nakala ya Form ya sample ya scholarship ya China Scholarship Council ambayo ni plain haijajaza,
- kisha print hiyo form halafu chukua kalamu nyekundu koleza kwa ruler sehemu inayohitaji uandike passport name na passport number.
- Baada ya hapo, Andika barua ya kurequest kuwa unahitaji kupatiwa passport ili uweze kuendelea na maombi yako ya scholarship utaje kabisa na tarehe ya wakati passport utaihitaji.

Ukijumlisha na viambatanisho vyake vifuatavyo;

1. **Barua ya serikali ya mtaa utambulisho/ au barua ya utambulisho kutoka kazini kwako ikiwa na picha yako**
2. **Kopi ya ID ya taifa yako.**
3. **Kopi ya vyeti vyako vya shule**
4. **Kopi ya cheti cha kuzaliwa cha Mzazi (Ukiweka kimoja au vyote sio mbaya.. Kama hana Cheti unaweza kwenda kwa Mwanasheria kuomba Affidavit) Pamoja na cheti chako cha kuzaliwa**
5. **Application form ambayo ulifanyia maombi ktk system uhamiaji (Online) Na ulilipia (20,000)**
6. **The remaining amount 130,000 ukienda kusubmit. Ambapo jumla itakuwa ni 150,000 pamoja ya hiyo amount ya namba 5.**

Fanyieni kazi hayo niliyowatumia hapo juu, Labda kikwazo tu kiwe hiyo ID ya taifa kwa mtu ambaye hauna, ila the rest ni kupambana tu mpaka unaipata.

Ikumbukwe ni njia rahisi sana hiyo na ukienda full umejikamilishaa kwa kila kitu nyuma ya pazia kama hivyo unajikuta siku unakanyaga uhamiaji ni kufanya process za kusubmit na siku unayorudi ni ya kubeba passport yako tu.

**UKIENDA USISAHAU BEBA NA HIZO ORIGINAL CERITIFICATE ZAKO ZOTE i.e KUZALIWA, VYA SHULE, VYA WAZAZI, ID ZOTE**

OFISI ZA UHAMIAJI KWA UNAYEANZA SASA NENDA **DIRECT KURASINI, ULIZIA DIRECTION** KWA WENZENU, PEANENI MAELEZO YA KUTOSHA, MFIKE KWA WAKATI NA MUWAHI (DAR ES SALAAM)-KAMA HAWAJAHAMA.